# Uchumi na BIASHARA



11

UDHIBITI WA EWURA ULIVYOLINUFAISHA TAIFA



Aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (mwenye miwani) akishirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk Vincent Anney na Mkuu wa Wilaya ya Butiama, Bi Anarozy Nyamubi kuteketeza nyavu haramu zilizokamatwa na kikosi kazi maalumu alichokiunda hivi karibuni katika wilaya ya Musoma.(Picha ya mtandao).

## Sababu za uvuvi haramu kutoisha Ziwa Victoria

Na Dk Vicent Anney

TANZANIA ni nchi iliyobarikiwa sana na Mwenyezi Mungu kulinganisha na nchi nyingi barani Afrika kutokana na kuwa na rasilimali nyingi katika maeneo mbalimbali.

Imebarikiwa kuwa ni bahari, maziwa, mito misitu, madini, mifugo, wanyama mwitu, nyuki na kadhalika.

Katika makala haya nitazungumzia zaidi rasilimali zinazopatikana majini ambazo ni sehemu ya uchumi wa bluu (blue economy).

Mbali ya maji haya tuliyo nayo kutumika kama njia ya usafiri, kumwagilia mashamba na kuzalisha umeme, lakini pia tunapata samaki kupitia shughuli za uvuvi na hivyo maji kuwa kiwanda kikubwa cha kuzalisha ajira.

Katika makala haya ambayo nitajikita zaidi katika suala la uvuvi haramu na madhara yake, yanatokana na uzoefu wangu wa miaka minne katika kushughulikia mapambano ya uvuvi haramu katika wilaya ya Musoma ambayo ina eneo kubwa la Ziwa Victoria.

Ziwa hili ni mgodi au kiwanda tulichopewa na Mwenyezi Mungu ili tukitumie kwa ajili yetu na vizazi vijavyo. Ninasema ni mgodi kwa sababu kila mmoja anaweza kuutumia mgodi huu bila kuwa na gharama kubwa za uwekezaji.

Ziwa hili linatoa samaki wa aina mbalimbali ambao wanavuliwa na wananchi bila kushiriki katika kuwalisha wala kuwajengea mabanda kama mifugo wengine. Anachofanya mtu ni kuandaa tu zana zake za uvuvi, basi.

Ziwa Victoria ambalo pia linakwenda hadi Uganda na Kenya ni zawadi ya Mwenyezi Mungu kwa wananchi wa mikoa ya Mara, Mwanza, Kagera, Geita, Simiyu na Tanzania kwa ujumla wake.

Lakini zawadi hii imekuwa kama laana kwa sisi wananchi wenyewe. Badala ya kuitunza ili tuendelee kunufaika na viumbe waliomo, tumekuwa waharibifu wakubwa. Hapa sizungumzii uharibifu wa mazingira ya ziwa bali uvuvi haramu utakaomaliza samaki ziwani.

Kwa nini suala la uvuvi haramu limeshindikana kuisha kabisa katika maziwa na mito ya Tanzania? Kwa muda wa miaka mitano ya kazi yangu ya ukuu wa wilaya nimebaini kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kubadili mkakati wa kupambana na uvuvi haramu katika maziwa makuu ya Tanzania

Inaendelea Uk. 13

Scanned with CamScanner

Mtanzania Tarehe 10/11/2020
Uk.8



# Serikali yaombwa kukuza fursa za mabondo ya samaki

Na YOHANA PAUL
-MWANZA

WIZARA ya Mifugo Uvuvi na Wizara ya Viwanda na Biashara,imeombwa kuunda sera rafiki zitakazosaidia kukuza fursa ya biashara ya mabondo ya samaki ambayo yametajwa kuwa na thamani kubwa kuliko minofu ya samaki.

Rai hiyo, ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita mkoani hapa na Mwenyekiti Mtendaji wa Taasisi isiyokuwa ya kiserikali ya Fishers Union Organisation (FUO), Juvenary Matagili inayojishughulisha na kutoa elimu ya afya, mazingira na teknolojia mbadala ya uvuvi kwa wavuvi, alipokuwa anazungumuza na waandishi wa habari ofisi kwake.

Alisema ana imani na sera za serikali ya awamu ya tano hususani ilivyojikita kukuza uchumi kupitia viwanda lakini bado inapaswa kuweka sera rafiki ili kukuza biashara ya mabondo ya samaki kwani wavuvi wengi wamekuwa wakiuza samaki viwandani kwa thamani ya minofu pekee, huku mabondo yakiwa hayaangaliwi.

Alisema taarifa ilizonazo, mabondo yana thamani kubwa kuliko hata minofu ya samaki ingawa bado biashara hiyo adhimu haitazamwi kwa ukubwa, ambayo iwapo ingewekewa sera na usimamizi mzuri huenda ingeliingizia pesa nyingi taifa pamoja na kuwafaidisha wavuvi wenyewe.

Alishauri iundwe bodi ya uvuvi itakayohusisha siyo wasomi peke bali pia wavuvi wakubwa na wadogo ambao watasaidia kutoa maoni yao jinsi gani biashara ya mabondo inaweza kuwa na tija zaidi tofauti na ilivyo sasa ambapo hakuna muongozo maalumu wa biashara hiyo kiasi cha kupelekea wavuvi wengi wanapouza samaki viwandani kutolipwa thamani ya bondo kitu ambacho siyo sawa.

Alisema uwepo wa taasisi itakayosimamia haki za wavuvi itaweza kuwainua kiuchumi kwa kuwa kabla ya kuuza samaki yatafanywa makadilio ya thamani ya bondo na minofu ili mwisho wa siku mvuvi apate pesa inayoendana na thamani ya mzigo aliotyoa.

- PICHA: MPIGAPICHA WETU



**UZINDUZI:** Meneja wa Kiwanda cha Konyagi, Aranyaeli Ayo (kulia) akikata utepe kuzindua mchezo wa bahati ya mawakala wa kampuni hiyo, Dar es Salaam juzi ambapo mawakala 4 kila mmoja amejishindia pikipiki za matairi 3. Kushoto ni Meneja Usimamizi wa Kanda za Mauzo wa TDL, Mwesige Mchuruza.

Scanned with CamScanner

# Wizara yakarabati mabwawa mawili

**Longido.** Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel amesema Serikali inatumia zaidi ya Sh900 milioni kukarabati mabwawa mawili ya kunyweshea mifugo ya Narakauo lililopo wilayani Simanjiro, mkoani Manyara na bwawa la Kimokuwa lililopo wilayani Longido mkoani Arusha.

Profesa Gabriel alieleza hayo juzi alipokuwa katika ziara ya kukagua maendeleo ya ukarabati wa mabwawa hayo.

Akizungumza na wafugaji baada ya ziara hiyo, Prof. Gabriel alisema bwawa la Narakauo limetengewa milioni 413 wakati bwawa la Kimokuwa limetengewa milioni 511.9.

Alisema ukarabati huo ni utekelezaji wa maelekezo aliyoyatoa Rais John Magufuli aliyotoa hivi karibuni mkoani Manyara.

**(Mwandishi Wetu)**

Scanned with CamScanner